**18-At-Tafkhiym Na At-Tarqiyq (Kutamka Herufi Kwa Unene Au Wembamba)**

**التَّفْخِيمُ والتَّرْقِيق**

**التَّفْخِيم At-Tafkhiym - Kufanya Nene Au Nzito (mdomo kujaa)**

Maana yake: Kufanya nene au kuitamka kwa uzito.

Katika hukmu ya Tajwiyd ni kuitamka herufi kwa kuifanya nene na nzito nayo hupatikana kwa kupandisha ulimi juu kwenye sakafu ya kinywa hadi kukifanya kinywa kijae inapotamkwa herufi.

**التَّرْقَيق At-Tarqiyq - Kufanya Nyembamba au Nyepesi**

Maana yake: Kufanya nyembamba au nyepesi.

Katika hukmu ya Tajwiyd ni kuitamka herufi kuifanya nyembamba na nyepesi, nayo hupatikana kwa kuteremsha ulimi uwe mbali na sakafu ya kinywa (uwe chini) hadi kukifanya kinywa kisijae.

Tafkhiym na tarqiyq katika herufi za hijaaiyyah ziko katika hali tatu:

**1. تَفْخِيمُ دآئماً Tafkhiym daima**

Ni herufi za اْلإسْتِعْلاء (al-isti'laa - kupaa juu) nazo ni; **خص ضغط قظ** . Uzito wa tafkhiym hauko sawa katika herufi za اْلإسْتِعْلاء (al-isti'laa) kwa sababu herufi **ط ض ص ظ** zina swiffah ya **الإطْباق** (al-itwbaaq -kufunga) ambazo ulimi unagandamiza sakafu ya kinywa. Hivyo basi huwa ni nzito zaidi kuliko herufi خ غ ق ambazo ulimi, sehemu yake ya mbele unalala chini ya kinywa.

Pia herufi za **تَفْخِيم** (tafkhiym - nzito) hupishana uzito wake kutegemea na daraja ya *i'raab* zake. Kwanza huwa nzito zinapobeba fat-hah na zikafatiwa na ألِف (alif) kisha fat-hah isiyo na ألِف (alif), kisha dhwammah, kisha sukuwn na mwisho kasrah.

| Inapobeba kasrah | Inapobeba sukuwn | Inapobeba dhwammah | Inapobeba fat-hah |
|---|---|---|---|
| مُّبۡصِرُونَ | يَسۡتَضۡعِفُ | ٱلۡقُرۡءَانُ | ٱلضَّآلِّينَ |
| ٱلۡمُسۡتَقِيمَ | مَّغۡفِرَةٌ | طُوبَىٰ | طَآئِفٌ |
| ٱلۡعَظِيمُ | خَلَقۡنَٰكُمۡ | ٱلۡخُلَطَآءِ | خَٰلِدِينَ |

### 2. تَرْقِيقُ دآئماً Tarqiyq Daima

Ni herufi zote zilizobakia za إسْتِفال (istifaal -kuinamisha) isipokuwa herufi mbili ر na ل. Herufi zilizo na swiffah ya إسْتِفال (istifaal) zitamkwe kwa kuteremsha ulimi ili zibakie kuwa ni تَرْقِيقُ (tarqiyq - nyepesi) mifano:

فَأَمَّا مَنۡ أُوتِيَ كِتَٰبَهُۥ بِيَمِينِهِۦ ﴿٧﴾ [1]

وَنَفۡسٖ وَمَا سَوَّىٰهَا ﴿٧﴾ [2]

إِنَّهُۥ هُوَ يُبۡدِئُ وَيُعِيدُ ﴿١٣﴾ [3]

### 3. بَيْنَ التَّفْخِيمُ وَالتَّرْقِيق Baina ya Tafkhiym na Tarqiyq

Ni herufi ambazo hutokea zikawa baadhi ya wakati zikawa ni تَفْخِيمُ (tafkhiym – nzito), na wakati mwengine zikawa ni تَرْقِيقُ (tarqiyq - nyepesi) kutegemea na hali inayokutana nazo.

---

[1]Al-Inshiqaaq (84: 7)
[2]Ash-Shams (91 : 7)
[3]Al-Buruwj (85: 13)

i) Alif ( ا ) ya madd

ii) Laam ( ل ) ya Lafdhw Al-Jalaalah (ﷲ)

iii) Raa ( ر )